Ukweli Kuhusu Wokovu

Na R.S Neaville

Sehemu ya Kwanza: Kipawa cha Bure

Jambo la kwanza ambalo mtu anastahili kujua kuhusu wokovu ni kwamba unakuja kupitia kwa mwana wa mungu Yesu Kristo.

> Yohana 14:6 Yesu akamwambia,
> mimi ndimi njia na kweli, na uzima;
> mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.

Hakuna njia nyingine ya kuokoka. Jambo la pili ambalo mtu anastahili kufahamu ni kwamba wokovu ni kipawa cha bure kutoka kwa mungu. Hakiwezi kununuliwa

> Warumi 5: 8 Bali Mungu aonyesha pendo
> lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa
> Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali
> wenye dhambi.
> 9. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki
> katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa
> yeye.
> 10. Kwa maana, ikiwa tulipokuwa adui
> tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya mwana
> wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa
> tutaokolewa katika uzima wake.

11**.** Wala si hivyo tu; ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye sasa tumeupokea huo upatanisho.
12. Kwa hivyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi.
13. Maana kabla ya sheria dhambi ilikuwamo ulimwenguni, lakini dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria,
14. Walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa, nayo iliwatawala wala hata wao wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la Adamu, aliye mfano wake yeye atakayekuja.
15. Lakini **karama** ile haikuwa kama lile kosa; kwa maana ikiwa kw a kukosa kwake yule mmoja wengi walikufa, zaidi sana neema ya Mungu, na kipawa kilicho katika **neema** yake mwanadamu mmoja Yesu Kristo kimezidi kwa ajili ya wale wengi.
16. Wala kadiri ya yule mtu mmoja aliyefanya dhambi si kadri ya kile **kipawa**; kwa maana hukumu ilikuja kwa njia ya mtu mmoja ikaleta adhambu; bali kwamba ya **neema** ilikuja kwa ajili ya makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki.
17. Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja, mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile **kipawa cha haki,** watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo)
18. Basi tena, Kama kwa kosa moja, watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika

kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima.

Kipawa hiki tulipewa tulipokuwa bado maadui wa Mungu. Sio kwamba ambalo linaonyesha kwamba sisi tunastahili. Ni lazima tukikubali kupitia kwa imani.

Jambo la tatu ni kwamba wokovu ni kwa neema ya mungu (kibali ambacho hatungenunua kutoka kwa Mungu, ambacho yetu alitununulia) kupitia kwa imani katika kafara. Ni kwa kuonyesha imani kuwa kafara ya Yesu itositosha kutuleta kwa njia iliyo sawa na Mungu Baba. Nikupitia kwa imani hii tunaweza kuzaliwa katika familia ya Mungu. Kwa imani ndani ya kafara ya Yesu tunaweza kuzaliwa tena katika maumbile isiyo halibika ya roho.

> Yohana 1:12 Bali wote walio mpokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake;
> 13. Waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu.
> 14. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.

Waraka wa 1 wa Petro 1: 21 ambao kwa yeye mmekuwa wenye kumwamini Mungu, aliyemfufua katika wafu akampa utukufu; hata imani yenu na tumaini lenu liwe kwa Mungu
22. Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na urafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo
23. Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele.

Wangatia 4:4 Hata ulipo wadia utimilifu wa wakati Mungu alimtuma mwanawe ambaye amezaliwa chini ya sheria,
5. Kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana.
6. Na kwa kuwa ninyi mumekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani Baba.
7. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana, na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu.

Waefeso 1:3 Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo.
4**.** Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu

hatia mbele zake katika pendo:
5. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawa sawa na uradhi wa mapenzi yake.
6. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo mpendwa.
7. Katika yeye huyo kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, hali hii ya kuwa wana ni kwa neema ya Mungu kupitia kwa imani ndani ya kafara na ufufuo wa Yesu.

Na kwa hivyo hapa ndipo wokovu wetu huanzia. unatolewa kwa watu wote kama kipawa cha bure kutoka kwa Mungu. Kile tunachotakiwa kufanya ni kukikubali tu. Lakini tunakikubali vipi haswa? Soma vifungu vifuotavyo kwa makini.

Yohana 1:12 Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.

Yohana 3:15 Ili kila mtu aaminiye awe na uzima wa milele katika yeye.
16. Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwana wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele.

17. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu lakini bali ulimwengu uokolewe katika yeye.
18. Amwaminiye yeye hahukumiwi asiye amini amekwisha kuhukumiwa kwa sababu hakuamini jina la mwana pekee wa Mungu.

Warumi 10:6 Bali ile haki ipatikanayo kwa imani yanena hivi, msiseme moyoni mwako, ni nani atakayepanda kwenda mbinguni? (Yaani, ni kumleta Kristo chini)
7. Au, ni nani atakaye shuka kwenda kuzimuni? (Yaani, ni kumleta Kristo juu, kutoka kwa wafu)
8**.** Lakini yanenaje? Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako, na katika moyo wako; yaani, ni lile neno la imani tulihubirilo;
9. Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako yakuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwake ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka
10. Na maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.
11. Kwa maana andiko la nena, kila amwaminiye hatatahayarika. hatahaibika

Tunakubali kipawa cha bure cha wokovu kupitia kwa imani!

Lakini imani ni nini haswa? Hapa ndipo wengi huchanganyikiwa.

Sehemu inayofuata inashugulikia imani. Hapa ndipo mtoto wa Mungu anastahili kuwa makini.

Maswali ya Marudio

1. Mungu alionyeshaje upendo wako tulipokuwa tungali wenye dhambi?
2. Neema ni nini? Jadilianeni hili na darasa
3. Kipawa cha bure cha wokovu kimetolewa kwa nani?
4. Imani yetu iko ndani ya nini?
5. Kuna wokovu wowote bali kwa kutolea kwa imani

Sehemu ya Pili: Imani ni nini?

Kama tulivyoonyesha hapo mbeleni wokovu huu mkubwa ulikuja kwetu kupita kwa imani. Unatolewa kwa yeyote na wote wanaoamini. Lakini kusadiki kunahusu nini haswa? Imani ni nini?

Waebrania 11.

1. Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasionekana.
2. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa.
3. Kwa imani twafahamu yakuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.
4. Kwa imani habili alimtolea Mungu dhabuhu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hivyo, alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hivyo ijapokuwa amekufa, angali akinena.
5. Kwa imani Henoko alihamishwa; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu.

6. Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wautafutao.
7. Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasionekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake.
Na kwa hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.
8. Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopata kuwa urithi. Akatoka asijue aendako.
9. Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake akikaa katika hema pamoja naye wa ahadi ile ile.
10. Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.
11. Kwa imani hata Sara mwenyewe alipokea uwezo wa kuwa na mimba, alipokuwa amepita wakati wake; kwa kuwa alimhesabu yeye aliyeahidi kuwa mwaminifu.
12. Kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, watu wengi

kama nyota za mbinguni na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika.
13. Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakziona tokea mbali na kuzishangilia na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi.

Sehemu ya Pili: Imani ni nini?

Kama tulivyoonyesha hapo mbeleni wokovu huu mkubwa ulikuja kwetu kupita kwa imani. Unatolewa kwa yeyote na wote wanaoamini. Lakini kusadiki kunahusu nini haswa? Imani ni nini?

Waebrania 11.
1. Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasionekana.
2. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa.
3. Kwa imani twafahamu yakuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri.
4. Kwa imani habili alimtolea Mungu dhabuhu iliyo bora kuliko Kaini; kwa hivyo, alishuhudiwa kuwa ana haki; Mungu akazishuhudia sadaka zake, na kwa hivyo ijapokuwa amekufa, angali akinena.
5. Kwa imani Henoko alihamishwa; maana kabla ya kuhamishwa alikuwa ameshuhudiwa kwamba amempendeza Mungu.

6. Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wautafutao.
7. Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasionekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake.
Na kwa hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani.
8. Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopata kuwa urithi. Akatoka asijue aendako.
9. Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake akikaa katika hema pamoja naye wa ahadi ile ile.
10. Maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi, ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.
11. Kwa imani hata Sara mwenyewe alipokea uwezo wa kuwa na mimba, alipokuwa amepita wakati wake; kwa kuwa alimhesabu yeye aliyeahidi kuwa mwaminifu.
12. Kwa ajili ya hayo wakazaliwa na mtu mmoja, naye alikuwa kama mfu, watu wengi

kama nyota za mbinguni na kama mchanga ulio ufuoni, usioweza kuhesabika.

13. Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakziona tokea mbali na kuzishangilia na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi.

kwa misumeno walibarikiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, walikuwa wahitaji, wakiteswa, wakitendewa mabaya,
38. (Watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao) walikuwa wakizunguka – zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi.
39. Na watu hao wote wakisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawa kuipokea ahadi.
40. Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora; ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.

Watu hawa wote wa imani walipokea vivuli ama picha za ahadi ya kweli ya wokovu. Wokovu katika utimilifu wake ni ule ufufuo wa wafu. Hakuna hata mmoja wao aliyepokea hayo. Waliona tu kupitia kwa picha ama vivuli na wakaikaribisha kwa mbali. Walichofanya haikuwa kwa sababu ya kile wangepokea katika ulimwengu huu. Ilikuwa ni imani iliyoundwa juu ya u milele na ufufuo wa ukamilifu

unaokuja tu kupitia kwa Yesu Kristo. Kuwa na hali ya uana kwetu kupitia kwa imani sio tofauti sana na yao. Tuna ahadi ya ufufuo huo mkuu. Ndio tumaini ya injili hii. Ndio ukamilifu wa wokovu wetu na wao.

> Waebrania 11:39 Na watu hao wote wakiisha kushuhudiwa kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi.
> 40. Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.

> Warumi 8:21 Kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu.
> 22. Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa.
> 23. Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukitazamia kufanywa wana, yaani ukombozi wa mwili wetu.
> 24. Kwa tuliokolewa kwa faraja; lakini kitu kilichotarajiwa kikionekana, hakuna faraja tena. Kwa maana ni nani anayekutarajia kile akionacho?
> 25. Bali tukikitarajia kitu tusichokiona twakingojea kwa sababu.

Imani yetu katika Kristo ndio dhihirisho la tulichoahidiwa. Ndio tumaini letu katika injili hii. Ni imani katika kitu ambacho hakijaonekana bado. Ni kitu ambacho bado hatuna kuwa wana ndani ya Yesu si roho bali pia miili yetu. Hii ndio ukamilifu wa wana wetu. Huu ndio wokovu ambao tunasimama kwa imani kwa ajili yake na kungojea kwa kutarajia kuona. Wokovu wetu ni sawa na wa mababu zetu katika imani. Ni ufufuo wa waliokufa. Paulo aliliambia kanisa la wafilipi.

> Wafilipi 3:10 Ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake.
> 11. Ili nipate kwa njia yoyote kuifikia kiyama ya wafu.
> 12. Si kwamba nimekwisha kufika, au mimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishuka lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu.
>
> Wafilipi 3:17 Ndugu zangu, mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi.
> 18. (Maana wengi huenenda, ambao nimewaambiene mara nyingi habaeri zao, na sasa nawaambia hata kwa machozi, kuwa ni adui wa msalaba wa Kristo:

19. Mwisho wao ni uharibifu, mungu wao ni tumbo, utukufu wao ni katika fedheha yao, wanao mambo ya duniani.
20. Kwa maana sisi wenyenji wetu uko mbinguni kutoka huko tunamtazamia huyo mwokozi, Bwana Yesu Kristo.
21. Atakaye ubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitisha vitu vyote viwe chini yake.

Huu ndio mwisho wa wokovu wetu kwa imani. Ahadi za Mungu kupitia kwa neno na kuwekwa Roho ndani yetu ni dhibitisho la jambo hili. Huu ndio msingi wa imani ambayo kwayo sasa twasimama ndani ya neema.

1. Pasipo imani haiwezekani kumfurahisha Mungu.

Waebrania 11:6 Pasipo imani haiwezekani kumfurahisha Mungu, kwa maana mtu amwendeaye lazima amini kwamba yeye yuk o, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.

Imani ni jambo la kiroho wala sio mwili pasipo hiyo hapana ushirikiano na Mungu.

Ikiwa haipo hapana wokovu . Kile tulichonacho ndani ya Yesu Kristo ni kupitia kwa imani. Imani si jambo la wakati mmoja. Ni kazi ya kila wakati katika uhusiano wetu na Mungu. Imani ikiisha vile vile tuamaini la wokovu. Mfano mzuri ni wakati Petro alitembea juu ya maji. Wakati wote macho yake yalipokuwa kwa Yesu alikuwa sawa. Alipoangalia upepo alizama. Hii inaonyesha imani unaofanya kazi. Inaonyesha pia matokeo ya kukosa imani.

> Mathayo 14: 27 Mara Yesu alinena akawaambia jipeni moyo ni mimi, msiogope.
> 28. Petro akamjibu, akasema, Bwana ikiwa ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji.
> 29. Akasema, njoo. Petro akashuka chomboni, akaenda kwa miguu juu ya maji, ili kumwendea Yesu.
> 30. Lakini alipouona upep, akaogopa, akaanza kuzama, akipiga yowe, Bwana niokoe.
> 31. Mara Yesu akaonyesha mkono wake, akamshika, akamwambia, ewe mwenye imani haba, mbona uko na shaka?
>
> Warumi 1:16 Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu uweza wa Mungu

uuletao wokovu, kwa kila aaminiye , kwa Muyahundi kwanza na kwa Myunani pia.
17. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.

Hivi ndivyo tunatakiwa kuishi …….kutoka imani hadi imani. Kwa maneno mengine imani ya kuendelea. Haiwezi kusimama ikisimama vile vile tumaini letu.

Warumi 1: 17 Lakini iwapo matawi mengine yamekatwa, na wewe mzeituni mwitu ulipandikizwa kati yao, ukawa mshirika wa shina la mzeituni na unono wake.
18. Usijisifu juu ya matawi yale, au ikiwa wajisifu, si wewe ulichukuaye shina, bali ni shina likuchualo wewe.
19. Basi utasema, matawi yale yalikatwa kusudi ili nipandikizwe mimi.
20. Vema yalikatwa kwa kutoamini kwao na wewe wasimama kwa imani yako. Usijivune, bali uogope.
21. Kwa maana ikiwa Mungu hakuyaachia matawi ya asili, wala hatakuachia wewe.
22. Tazama, basi, wema na ukali wa Mungu kwa wale walianguka, ukali, bali kwako wewe wema wa Mungu, ukikaa

katika wema huo; kama sivyo , wewe nawe utakatiliwa mbali.

Hii ndio injili yetu. Pasipo imani hakuna wokovu. Hatuendi kulingana na kile tulichonacho mkonononi au kuona kwa macho yetu. Tuna na kuishi na kupumua katika ulimwengu wa roho kupita kwa imani.

2 Wakorintho 5:7 (maana twaenda kwa imani, si kwa kuona)

Wagalatia 3:13 Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti.
14. Ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie mataifa katika Yesu Kristo tupate kupokea ahadi ya roho kwa njia ya imani.
15. Ndugu zangu, nanena kwa jinsi ya kibinadamu. Lijapokuwa ni agano la mwanadamu, hata hivyo likiisha kuthibitika, hakuna mtu alibatilishaye wala kuliongeza neno.
16. Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Haseni, kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kama kwamba ni mmoja, kwa mzao wako, yaani Kristo.

17. Nisemalo ni hili; agano lililothibitishwa kwanza na Mungu, Torati iliyotokea miaka mia nne na thelathini baadaye hailitangui, hata kuibatilisha ili ahadi.
18. Kwa maana urithi ukiwa kwa sheria haiwezi tena kwa ahadi. Lakini Mungu alimkirimia Ibrahimu kwa njia ya ahadi.
19. Torati ni nini basi? Ilingizwa kwa sababu ya makosa, hata aje hiyo mzao aliyepewa ile ahadi, iliamriwa kwa utumishi wa malaika kwa mkono wa mjumbe.
20. Basi aliye mjumbe si mjumbe wa mmoja, bali Mungu ni mmoja.
21.Basi je! Torati haipatani na ahadi za Mungu? Hasha! kwa kuwa , kama ingalitolewa sheria iwezayo kuhuisha, lakini haki ingalipatikana kwa sheria.
22. Lakini andiko imeyafunga yote chini ya nguvu ya dhambi, makusudi hao waaminio wapewe ile ahadi kwa imani ya Yesu Kristo.
23. Lakini kabla ya kuja ile imani tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ije ile imani itakayofunuliwa.
24. Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani.
25. Lakini iwapo imani imekuja , hatupo tena chini kiongozi.

26. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu.

Ni wazi kutoka kwa maandiko kile tulicho nacho kuhusu wokovu ni kwa imani. Kupoteza imani ni kupoteza tumaini la wokovu. Nikukataa Kristo na kusulubiwa kwake. Imani yako nikuwa Mungu ataweka ahadi yake.

Waefeso 2:8 – 9 Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu ni kipawa cha Mungu.
9. Wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.

Wakolosai 1:18 Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.
19. Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae;
20. Na kwa yeye kulipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake, kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni
21. Na ninyi, mliokuwapo hapo kwanza mmefarkishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa.

22. Katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake; uli awalete ninyi mbele zake; watakatifu, wasio na manufaa wala lawama.
23. **Mkidumu tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi mkawa imara, msipogezwa na kuliacha tuamini la injili mliyosikia habari zake**, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu, ambayo mimi Paulo alikuwa mhudumu wake.

Ni ukweli wa kuhuzunisha kwamba kuna wale ambao wametupa imani yao ndani ya Kristo ….. na hivyo tuamini la kufufuka ndani yake.

1 Timotheo 4

1. Basi roho anena wazi wazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetai.
2. Kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe

2 Timotheo 3

1. Lakini ufahamu neno hili yakuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari.

2. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi. Wao wasio na shukrani, wasio safi.
3. Wasiopenda wakwao, wasiotaka kufanya suluhu, wazingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapenda anasa kuliko kumpenda Mungu.
5. Wenye mfano wa utaua, lakini wakikana nguvu zake; hao nao ujiepushe nao.
6. Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu na kuchukua mateka wanawake, wajinga wenye mizigo ya dhambi; waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi,
7. Wakijifunza siku zote; ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli
8. Na kama vile Yane na Yambre walivyopungana na Musa, vivyo hivyo na hawa wanapina na ile kweli ni watu walio haribika akili zao, wamekataliwa kwa mambo ya imani.
9. Lakini hawataendelea sana. Maana upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote, kama vile na upumbavu wa hao ulivyokuwa dhahiri.

Waebrania 10:35 Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu.

36. Maana ninahitahi saburi, ili kamba mkisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi.
37. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana yeye ajaye atakuja, wala hatakawia
38. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani naye akisita-sita , roho yangu haina furaha naye.
39**.** Lakini sisi hatuna muongozi mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu.

3. Imani ilionyeshwa kupita yale watu waliyoyatenda, sio Kwa walio kwisha kuamini.

Mathayo 24:45 Ni nani basi yule mtumwa mwaminifu mwenye akili ambaye bwana wake alimweka juu ya nyumba yake, awape watu chakula kwa wakati wake?
46. Heri mtumwa ambaye bwana wake ajapo atamkuta akifanya hivyo.
47. Amini nawaambieni atamweka juu ya vitu vyako vyote.
48. Lakini mtumwa yule mbaya akisema moyoni mwake, Bwana wangu anakawia.
49. Akaanza kuwapiga wajoli wake na kula na kunywa pamoja na walevi.

50. Bwana wake mtumwa huyo atakuja siku asiyodhania na saa asijua
51. Atakata vipande viwili, na kumwekea fungu lake pamoja na wanafiki ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.

Kama ulivyoonyeshwa bayana katika vifungu vilivyo hapo juu. Imani imedhihirika aminifu. Neno mwaminifu inamaanisha utii. Imani itajionyesha katika utii. Huwezi kuwa umejaa imani ama mwaminifu bila kuwa mtiifu. Tunda la imani ni kile unachotenda katika utii. Kama wewe si mtiifu huwezi kuzaa tunda linalofaa kwa imani. Imani huzaa matendo mema ya utii.

Waebrania 6:4 Kwa maana hao wamekwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni na kufanywa washirika wa roho mtakatifu.
5. Na kulionja neno zuri la Mungu na nguvu za zamani zijazo.
6. Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu. Kwa kuwa wamsulubisha mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.
7. Maana nchi inayonyimwa mvua inayoinyeshea mara kwa mara , na kuzaaa mbegu zenye manufaa kwa hao ambao kwa ajili yao yakuwa hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu:

8. Bali ikitoa mamba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.
9. Lakini wapenzi , ijapokuwa twanena hayo, katika habari zenu tumesadiki **mambo yaliyo mazuri zaidi na yaliyo na wokovu.**
10 Maana Mungu si mdhalimu hata aisahau **kazi** yenu, na pendo mlilolidhihirisha kwa jina lake, kwa kuwa mmewahudumia watakatifu na hata hivi sasa mngali mkiwa hudumia.

Tazama maneno yanayofanana ya Yesu kuhusu utii na kuzaa tunda.

Yohana 15
1. Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na baba yangu ndiye mkulima.

2. Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa.
3. Ninyi mmekuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia.
4. Kaeni ndani yangu nami ndani yenu, kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu, kadhalika nanyi msipokaa ndani yangu.

5. Mimi ni mzabibu, nyinyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake huyo huzaaa sana, maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.
6. Mtu asipokaa ndani yangu hutupwa nje Kama tawi na kunyauka, watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea.

Hata Kama ni shamba linakuza miiba au ni tawi lizilozaa tunda, tazama yote miwili itateketezwa. Hii ni picha ya kifo cha pili.

Ufunuo 20:11 Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa cheupe na yeye aketie juu yake ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana.
12. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi, na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.
13. Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwa ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadri ya matendo yake.

14. Mauti na kuzimu zikatupwa kwenye lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili yaani hilo ziwa la moto.
15. Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.

Picha hii haikosei. Pasipo imani, Mungu hafurahishwi. Pasipo na imani hapana tunda nzuri.

Yakobo 2:14: Ndugu zangu, yafaaa nini, mtu akisema ya kwamba anayo imani, lakini hana matendo? Je! Ile imani yaweza kumwokoa?
15. Ikiwa ndugu mwanamume au ndugu mwanamke yu uchi na kupungukiwa na riziki,
16. Na mtu wa kwenu akawaambia, enendeni lakini asiwape mahitaji ya mwili, yafaa nini
17. Vivyo hivyo na imani, isipokuwa na matendo, imekufa nafsini mwake.
18. Lakini mtu atasema, wewe unayo imani, nami ninayo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu.
19. Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja, watenda vema. Mashetani nao waamini na kutetemeka.
20. Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani pasipo matendo haizai?

21**.** Je, Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu.
22. Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale.
23. Maandiko yale yakatimizwa yaliyonenwa. Ibrahimu alimwamini Mungu ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu.
24. Mwaona kwamba mwanadamu huhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo yake, si kwa imani peke yake.
25. Vivyo hivyo na Rahabu, yule kahaba naye je! Hakuhesabiwa kuwa ana haki ya matendo, hapo alipowakaribisha wajumbe, akawatoa nje kwa njia nyingine.
26**.** Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa.

Ikiwa imani yako haina matendo sio imani ya kweli. Imani huonyeshwa kwa kila unachokitenda.

4. Hakuna yeyote kati ya wale waliosimama kwa imani yao waliopokea walichoahidiwa katika dunia hii. Walisimama kwa imani kwa kile wangekipokea baadaye. Wote walikuwa wakiutazamia ulimwengu huo mwingine.

walingojea kwa subira kwa Mungu atimize ahadi zake. Kile walichokuwa nacho ni kwa imani.

Waebrania sura ya 11 ni mfano mkuu wa haya. Tunapoendelea tutaweka kwa undani imani ya baadhi ya watakatifu wa Agano la kale.Tutaonyesha kile walichopokea na ni nini kwa kweli walikuwa wakitafuta. Tutaonyesha kwa undani vile vile jambo hili kutoka kwa agano jipya.Tutaonyesha kutoka kwa andiko kuwa imani yetu inafanya kazi kwa njia hiyo. Kwa ajili imani inadhihirika au kuonyeshwa kwa kivuli au kudhihirika kunakoonekana kwa ahadi za Mungu. Hebu tuangalie vile ilivyofanya kazi na Ibrahimu.

> Waebrania 11:8 Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako.
> 9. Kwa imani alikaa ugenini katika nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile.
> 10. Maana alikuwa akuitazamia mji wenye misingi ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.

Hapo Mungu alimwita Ibrahimu atoke kwa familia yake na nchi amwonyeshe nyingine iliyokuwa bora zaidi.
Ilianza kwa ahadi ilioonekana lakini mahali katika mazoezi ya kumfuata Mungu kwa imani ikawa ya kiroho.
Ibrahimu akaanza kuangalia kupitia kwa ahadi ilionekana kuona ile ya kiroho. Hili ndilo kusudi la ile inayoonekana inashuhudia ile ya kiroho. Imani ndio funguo inayoleta kupita kutoka huku hadi kwingine.
Paulo anatwambia haya katika Waruni sura ya kwanza.

> Warumi 1:16 Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.
> 17. Kwa maana haki ya Mungu, inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa. mwenye haki ataishi kwa imani.
> 18. kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu.
> 19**.** <u>Kwa kuwa mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yaonekana na kufahamika kwa kazi zake; yaani uweza wa milele na uungu wake; hata wasiwe na udhuru.</u>

Katika hali ya kuharibika tunaangalia yale yanayoonekana na kukosa kumtambua muumba. Katika njia ya imani tunaangalia kupitia kwa yanyoonekana kuona yale mambo ya kiroho yanasimamia. Tunamtambua Mungu anayefunuliwa kupitia kwayo. Hili ilitendeka kwa Ibrahimu. Katika hali ya kumfuata Mungu kwa imani akaanza kuona ahadi za milele badala ya zile zinazoonekana. Yale yanayoonekana kwake yalikuwa mambo yanayodhihirisha mambo ya kweli yaliyo ahidiwa.Ndio sababu hakukubali kuchukua hata kiasi cha ardhi cha kweka mguu ya nchini ya ahadi lakini alikaa kwenye hema.Isaka na Yakobo walifuata imani yake. Stephano aliona haya katika matendo ya mtume.

> Matendo ya Mitume 7:
> 1. Kuhani mkuu akasema; je! Mambo haya ndiyo yalivyo?
> 2. Naye akasema, ndugu zangu na baba zangu, sikilizeni: Mungu wa utukufu alinitokea baba yetu Ibrahimu, alipokuwa katika Mesopotamia; kabla hajakaa harani,
> 3. Akamwambia, toka katika nchi yako na katika jamaa zako, ukaende hata nchi nitakayo kuonyesha.
> 4. Ndipo alipotoka katika nchi ya Wakaldayo, akakaa Harani, akatoka huko baaada ya kufa babaye, Mungu akamhamisha mpaka nchi hii mnayokaa ninyi sasa.

5.Wala hakumpa urithi humu hata kiasi cha kuweka mguu, akaahidi kwamba atampa, iwe milki yake, naya uzao wake baadaye alipokuwa hana mtoto.

Waebrania 11:9 Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama katika nchi isiyo yake, akikaa katika hema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi pamoja naye wa ahadi ile ile.
10. Maana alikuwa akimtazamia mji wenye misingi ambao mwenye kuubuni na kuujenga ni Mungu.

Ibrahimu alitazama ya milele. Yeye na uzao wake wakiishi kwenye hema. Hema ni makao ya mda mfupi kama tunavyoishi katika hema au "hema ya makutano" ya mwili huu. Ni ya muda maana tunatazamia mji kama ule Ibrahimu aliutazamia. Tunatazamia makao yetu ya milele katika mji ambao ni kufufuka.

2 Wakorintho 5:
1. Kwa maana twajua ya kuwa nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa tunalo jengo litokalo kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni
. 2. Maana katika nyumba hii twaungua, tukitamani sana kuvikwa
kao letu litokalo mbinguni.

3. Ikiwa tukiisha kuvika hatutaonekana tu uchi
4. Kwa sababu sisi tulio katika maskani hii twaugua, tukilemewa, si kwamba twataka kuvuliwa, bali kuvikwa, ili kitu kile kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima.
5. Basi yeye aliyetufanya kwa ajili ya neno lilo hilo ni Mungu, aliyetupa arabuni ya roho.

Angalia sasa mtoto wa ahadi wa Ibrahimu.Isaka alikuwa mwana wa ahadi wa kweli? Au alikuwa tu dhihirisho la ahadi iliyozungumza kuhusu Kristo Yesu?

Waebrania 11: 17 Kwa imani Ibrahimu alipojaribiwa, akamtoa Isaka awe dhabihu; na yeye alijezipokea hizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee.
18**.** Naam, yeye aliyeambiwa, katika Isaka uzao wake utaitwa.
20. <u>Akihesabiwa ya kuwa Mungu aweza kumfufua hata kutoka kwa kuzimu; akampata tena toka huko kwa mfano.</u>

Isaka ni mfano au kivuli cha mtoto wa kweli ambaye Ibrahimu angebarikiwa kupitia. Yesu alikuwa mbegu ya kweli ya Ibrahimu. Alikuwa mbegu iliyozaliwa ya umilele na sio ya muda. Ibrahimu alimsalimia na ahadi ya kufufuliwa kutoka mbali

Wagalatia 3. Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa uzao wake. Hasemi Kwa wazao, kana kwamba Ni wengi, Bali kana kwamba Ni mmoja Kwa mzao wako, yaani Kristo.
17. Nisemalo ni hili, agano lililothibitishwa kwanza na Mungu, torati iliyotokea miaka mia nne na thelathini baadaye hailitangui, hata kuibatilisha ile ahadi.
18. Kwa maana urithi ukiwa kwa sheria, hauwi tena kwa ahadi, lakini Mungu alinikirimia ibrahimu kwa njia ya ahadi.

Kwa hivyo ahadi inayoonekana sio ile Ibrahimu alikuwa akiitazama. Alizipokea tu kama ishara ya ahadi bora zaidi ambayo Mungu angeleta kupitia Yesu.
Kwa hakika mwandishi wa waebrania anatwambia eti Ibrahimu alikufa bila kupokea kile alichoahidiwa. Aliishi kupata Isaka lakini ni yesu alikuwa akiitazamia.

Waebrania 11: 13 Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia, na wasafiri juu ya nchi.
14. Maana hao wasemao maneno kama hayo waonyesha wazi kwamba wanatafuta nchi yao wenyewe.
15. Na kama wangalikumbuka nchi ili waliyotoka wangalipata nafasi ya kurejea.

16. Lakini sasa waitamani nchi iliyo bora, yaani ya mbinguni. Kwa hiyo Mungu haoni haya kuitwa Mungu wao, maana amewatengenezea mji.

Waebrania 11: 33 Ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa vya simba.
34.walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga. Walitumia nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni.
35. wanawake wakipokea wafu wao waliofufuliwa. Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa, wasikubali ukombozi, ili wapate ufufuo ulio bora.
36**.** Wengine walijaribiwa kwa dhihaka na mapigo, naam, kwa mafungo na kwa kuwa gerezani;
37. Walipigwa kwa mawe, walikatwa kwa musueno, walijaribiwa, waliuawa kwa upanga; walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi; walikuwa wahitaji, wakiteswa wakitendewa mabaya.
38. (Watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao), walikuwa wakizunguka – zunguka katika nyika na katika milima na katika mapango na katika mashimo ya nchi.

39. Na watu hao wote wakiishi kushuhudia kwa sababu ya imani yao, hawakuipokea ahadi.
40. Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.

Mashujaa wote wa imani walikufa wakitazamia kufufuliwa katiaka Kristo yesu. Kila walichokipokea kama baraka zinazoonekana zilikuwa ishara kwao za ahadi ambazo ni za milele. Sisi pia tungali kupokea ufufuo huu. Ndilo tumaini letu sisi na wao pamoja tutaipokea Kristo atakaporudi.

1 wakoritho 15: 16 Naam, na sisi tumeonekana kuwa mashahidi wa uongo wa Mungu; kwa maana tulimshuhudia Mungu ya kuwa alimfufua Kristo, ambaye hakumfufua, ikiwa wafu hawafufuliwi.
16. Maana kama wafu hawafufuliwi, Kristo naye hakufufuka, imani yeni ni bure; mngalimo katika dhambi zenu.
18. Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea.
19. Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu maskini kuliko watu wote.
20. Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala.
21. Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu kadhalika na kiyama ya wafu lilitetwa na mtu.
22. Kwa kuwa kama katika adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa.
24. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja.

Sasa hebu tuangalie njia ya imani kutoka kwa agano jipya.Tutaona kwamba ni sawa kwetu pia. Tunakile tulicho nacho cha wokovu kupitia kwa imani. Katika injili unapoona yote ya miujiza ya Yesu ni lazima tuanze kutambua kwamba yote haya yalikuwa kudhirishwa kwa muda kwa ahadi zake za milele. Zilikuwa vivuli tu ya kweli. FikirIa wale walioponywa na Yesu.

Viwete: picha ya wale ambao hawangeweza kutembea na Mungu kiroho.

Vipofu: Picha ya wale hawangeweza kuuona ufalme wa Mungu.

Viziwi: wale ambao hawangeweza kusikia kile roho alikuwa akisema.

Wenye ukoma: Wale ambao ni wachafu katika dhambi.

Waliopagawa mapepo: Wale ambao wamefungwa na shetani.

Wafu waliofufuliwa: Picha ya ufufuo wa milele.

Yesu kuwaponya hawa inaonyesha ahadi za mungu za ukombozi wa wanadamu wote.
Tena tunaona kwamba yale tunayoyaona ni picha ya muda ya ahadi za Mungu za milele. Kiini cha haya yote ni rahisi kile tulicho nacho sasa ni picha za wokovu zikidhihirisha ahadi za Mungu.Tulicho nacho sasa ni uhusiano wakiimani. Tulicho nacho sasa ni ahadi ya kufufuka. Mungu ametupatia kiasi ya roho wake. Kama uhakika kwamba tukiendelea katika uhusiano huu,

tutapokea yote ambayo tumeahindiwa Yesu atakaporudi. Ndio sasa tumeokoka …lakini ni kwa imani! Nikwa kile tunachokiamini au yule ambaye tunamwamini……sio yale tunayoyaona. Tunaamini Mungu na neno lake.

1 wakorintho 15**:** 22 Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, na kadhalika katika Kristo wote watahuishwa.
23. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja.

Waefeso 1:
9 Akiisha kutujulisha mapenzi alisukudia katika yeye huyo
10. Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu. Atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya dunia pia. Naam, katika yeye huyo.
11. Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawa sawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo kwa shauri mapenzi yake.
12. Nasi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli.Habari njema za wokovu wenu tena mmekwisha kumwamini yeye na kutiwa muhuri na roho yule wa ahadi aliye mtakatifu.
13. <u>Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.</u>

14. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake.

Wafilipi 3:20 Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia mwokozi, Bwana Yesu Kristo.
21. Atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufafana na mwili wake utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo uweza hata kuviitisha vitu vyote viwe chini yake.
1 Petro 1:3 Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tuamini lenye uzima kwa kufufuka kwake yesu Kristo katika wafu;
4. Tupate na urithi usioharibika, usio wa uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu.
5. Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu.
6. Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambu kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbali mbali.
7**.** Ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo niya thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo,

ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekana kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo.
8. Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini, na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu.
9. Katika kuupokea mwisho wa imani yenu, yaani, wokovu wa roho zenu.

Kile tulichonacho cha wokovu ni kushikamanishwa na Mungu kupitia kwa roho ambaho ililetwa kwetu na damu isiyo na hatia ya mwana mpendwa wa Mungu.Yesu amerejeshwa kushikamanishwa kwetu na muumba wetu. Yeye ndiye amani yetu na Mungu. Baadaye atarejesha mwili ili katika kuja kwake tutakamilika ndani yake. Hii ndiyo kuwa na uwana kama watoto wa Mungu.

Waruni 8:8 Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.
9. Lakini ikiwa roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati, mwili, bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yeyote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.
10. Na Kristo akiwa ndani yenu, mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi, bali roho yenu i hai, kwa sababu ya haki.
11. Lakini, ikiwa roho wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo

katika hali ya kufa kwa roho wake anayekaa ndani yenu.
12. Basi, kama ni hivyo, ndugu, tu wadani, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili.
13. Kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwatuka kufa; bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa roho, mtaishi.
14. Kwa kuwa wote wanaongozwa na roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.
15. Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu, bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hivyo *******, Aba, yaani Baba.
16. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu;
17. Na kama tu watoto, basi, tu warithi, warithi wa Mungu, warithio pamoja naye ilitupate na kutukuzwa pamoja naye.
18. Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu.
19. Kwa maaana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu.
20. Kwa maana viumbe vyote pia vilitiishwa chini ya ubatili, si kwa hari yake.
21. Kwa kuwa viumbe vyenyewe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu, hata viingie katika

utumwa wa uharibifu, hata utukufu wa watoto wa Mungu.
22. Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa.
23. Wala si hivyo tu; ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya roho, sisi pia tunaungua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanywa wana, yaani, ukombozi wa mwili wetu.
24. Kwa maana tuliokolewa kwa faraja, lakini kitu kilicho tarajiwa kikionekana hakuna faraja tena. Kwa maana ni nani anayekitarajia kile akionacho?

Roho wa Mungu aliye hai anadumu ndani yetu sasa kwa imani katika kafara ya Kristo. Yeye mwenyewe ndiye anayesimamia kwamba Mungu atakamilisha kile alichoanzisha. Ni kwa roho wake tunaweza kuitwa hata sasa watoto wa Mungu. Ni tamko la imani katika ahadi zake.

Wafilipi 1:6 Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu atamaliza hata siku ya Yesu Kristo

> Warumi 8:16 Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, yakuwa sisi tu watoto wa Mungu.
> 17. Na kama tu watoto, basi, tu warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo, naam, tuikiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.
> 18. Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wasasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu.
> 19. Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu.

Huu ndio wokovu wetu. Ni moja ya imani. Tunangojea kwa subira kwa tumaini kwa Mungu kukamilisha yote aliyoahidi. Tunatembea katika upatanisho huu wa roho na kupanda katika ufufuo kwa kuenenda kwa utii na kuendelea kwa imani. Kuendelea kwa nguvu ya roho wa Mungu aliye hai kupitia kwa Yesu na kafara yake na nguvu za kufufuka kwake. Hii ndio imani, tumaini letu, na injili yetu kama ibrahimu, hatuja pokea bado kile kimeahidiwa lakini kwa kuendeleza imani pamoja na Ibrahimu na wote mashujaa wa imani tutaweza.

> Waebrania 9:27 Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu.
> 28. Kadhalika Kristo naye, akisha kutolewa sadaka mara moja, azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya

pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu.

Waruni 13:10 Pendo haimfanyii jirani neno mbaya, basi pendo ndilo utimilifu wa sheria.
11. Naam tukiujua wakati, kwamba saa ya kuamka katika usingizi imekwisha kuwadia, Kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini.
12. Usiku ueendelea sana, mchana umekaribia, basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru.

Maswali ya Marudio

1. Ni mambo yapi manne ambayo Waebrania sura ya 11 inatwambia kuhusu imani?
2. Ni hakikisho gani kwetu kwamba Mungu atakamilisha wokovu wetu.
3. Kusadiki ni jambo la wakati mmoja? Jadilianeni hii darasani.
4. Wokovu unaweza kununuliwa?
5. Je, Imani huwa na matendo ili ionekane kwamba ni imani?

Kwa masomo mengine na yale ya redio katika MP3 na R.S Neaville tembelea http//prophetjournal.net. Tena tembelea masomo ya bibilia ya usiku katika sehemu ya ukristo: http://paltalk.com
Andikia R.S Neaville Kwa:
rsneaville@propheticjournal.net

Kitabu hiki kimetafsiriwa na Patmos Trust Fund:
patmostrust@yahoo.com

This booklet has been translated to Swahili Language by Patmos Trust Fund: patmostrust@yahoo.com with the permission of the Author